JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# SHERIA BULLETIN

Toleo la Sita

# UZINDUZI WA MAMA SAMIA LEGAL AID CAMPAIGN MANYARA

MAMA SAMIA Legal Aid Campaign



## YALIYOMO

02 | Mahabusu walalamikia vitendo vya Rushwa
03 | MSLAC yamaliza Mgogoro wa Ardhi
05 | Mbulu Wajitokeza Kuipokea MSLAC


## BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
Norah Uledi | William Mabusi | George Mwakyembe | Felix Chakila
**Wasanifu wa Kurasa:** Waziri Bosco | Richard Mwamakafu


CS CamScanner

# MAMA SAMIA LEGAL AID CAMPAIGN YAZINDULIWA MANYARA.

## HUDUMA KUTOLEWA KWA SIKU KUMI



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul akitoa hotuba ya ufunguzi akiwataka wananchi kutumia Huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign)*

**Na Lusajo Mwakabuku - WKS Manyara**

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Pauline Gekul amewataka wananchi kutumia Huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign), kupata haki zao pamoja na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Naibu Waziri Gekul alitoa wito huo Mei 23,2023 mjini Babati wakati akizindua kampeni hiyo kwa Mkoa wa Manyara, itakayotolewa bure kwa wananchi wote kwa siku kumi katika wilaya tano za mkoa huo.

Amesema kampeni hiyo inayosimamiwa na serikali kupitia wizara ya Katiba na Sheria, itasadia kuimarisha mfumo wa utoaji Huduma za msaada wa kisheria kuanzia Serikali Kuu Hadi Serikali za Mitaa.

Pia, Gekul amewaagiza viongozi wote kuanzia ngazi ya Vijiji, kuweka mfumo mzuri wa kushighilikia changamoto za kisheria zitakazoibuliwa wakati wa kampeni hiyo.

Aidha amesema wataalamu wa sheria kutoka wizara ya Katiba na Sheria watakuwepo katika wilaya zote tano za mkoa wa Manyara kwenye majimbo Saba kuwasikiliza wananchi kuanzia ngazi ya kata na kutoa elimu ya masuala mbalimbali yanayohusu Sheria.

Kampeni hiyo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara zingine, Wadau mbalimbali wa maendeleo na azaki za kiraia, imepewa jina la Mama Samia Legal Aid Campaign, ili kuenzi mchango wa Rais Dr. Samia Suluhu Hassan katika kutokomeza vitendo vya ukatili hasa kwa kina mama, watoto na makundi Maalum na kutoa nafasi ya msaada wa kisheria bure kwa wananchi wote.

Mwakilishi wa mkuu wa mkoa wa Manyara Kheri James ambaye ni mkuu wa wilaya ya Mbulu, amesema mkoa upo tayari kutoa ushirikiano ili wananchi waweze kupata huduma hiyo muhimu. Mwenyekiti wa chama cha Mapinduzi Pater Toima amempongeza na kumshukuru Rais kwa kuwakumbuka wanyonge wanaokosa haki zao kwa kutokujua sheria.



*Naibu Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu akitoa salamu za Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria aliyemuawakilisha katika uzinduzi huo.*



*Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Manyara Bwana Kheri James ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, akielezea utayari wa Mkoa katika kutoa ushirikiano ili wananchi waweze kupata huduma ya Mama Samia Legal Aid Campaign.*



CamScanner

# MAHABUSU WALALAMIKIA VITENDO VYA RUSHWA MANYARA

## Gekul aagiza watuhumiwa kuchunguzwa.



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul akifuatilia kwa makini taarifa inayotolewa na Kamishna Msaidizi wa Magereza ACP Nkonge Edwin alipofika gerezani hapo na timu ya wataalam wa Mama Samia Legal Aid Campaign.*

### Na Lusajo Mwakabuku - WKS Manyara

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul ameuagiza Uongozi wa Ofisi ya Mashtaka Mkoa wa Manyara pamoja na viongozi wa Jeshi la Polisi Mkoani humo kufanya uchunguzi juu ya tuhuma zilizotolewa na mahabusu na Wafungwa wa gereza la Babati Mjini dhidi ya askari na watumishi wa vyombo hivyo vya haki ambapo katika nyakati tofauti wameonekana kutumia nafasi zao kudai rushwa kwa malengo ya kukwepesha haki.

Tuhuma hizo zimetolewa tarehe 24/05/2023 wakati timu ya wataalam wanaoendesha Mama Samia Legal Aid Campaign ikiongozwa na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul ilipofika gerezani hapo kwa lengo la kutoa elimu pamoja na msaada wa kisheria kwa wafungwa na mahabusu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa kampeni hiyo kubwa iliyozinduliwa mwanzoni mwa mwaka huu ambayo itadumu kwa miaka mitatu mpaka 2026.



*Kamishna Msaidizi wa Magereza ACP Nkonge Edwin akisoma taarifa ya Gereza la Babati mara baada ya Mhe. Gekul na timu yake kuwasili katika gereza hilo kwa lengo la kutoa elimu na msaada wa kisheria.*

Akiambatana na wataalamu kutoka Ofisi ya Mashtaka, Tume ya haki za binadamu, Mrakibu wa Polisi wa Mkoa, Dawati la jinsia la polisi, Wanasheria na watumishi wengine kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Naibu Waziri Gekul alifika katika gereza la Babati na kufanikiwa kuongea na uongozi lakini pia na wafungwa na mahabusu waliokuwepo katika gereza hilo lengo likiwa ni kubaini changamoto za kisheria zikiwemo upatikanaji wa dhamana kwa wafungwa wanaostahili pamoja na namna kesi zao zinavyoendeshwa.

Timu ya wataalam wa Mama Samia Legal Aid Campaign ilipokewa na uongozi wa Gereza hilo ambapo pamoja na mambo mengine, Kamishna Msaidizi wa Magereza ACP Nkonge Edwin alimweleza Naibu Waziri kuwa moja kati ya vitu ambavyo gereza hilo limefanikiwa kuvitekeleza ni pamoja na kesi kusikilizwa kwa wakati kitu ambacho ni kilio kwa watu wengi walio vizuizini katika maeneo mengine huku akiainisha kasoro ndogondogo zikiwemo uchakavu wa vyombo vya usafiri katika kutoa huduma za wafungwa pamoja na kukataliwa kwa rufani zilizo nje ya muda.

Timu hiyo ya Mama Samia Legal Aid Campaign baada ya kuongea na uongozi wa Gereza iliingia ndani ya gereza na kuongeza na mahabusu pamoja na wafungwa ambapo elimu ya sheria ilitolewa jinsi mtu anavyokamatwa kituoni mpaka anapelekwa gerezani vitu vinavyotakiwa kufuatwa, Lakini pia mtaalam kutoka haki za binadamu alielezea haki za msingi za wafungwa wakiwemo gerezani ikiwemo haki ya dhamana kwa makosa yenye dhamana na pia Ofisa kutoka Ofisi ya Mashtaka akaongelea wajibu wa Ofisa wa mashtaka wa wilaya na muda uliopangwa kisheria wa kushughulikia kesi za watu walio vizuizini ambapo kwa kwa mkoa huu hali imeonekana kuwa shwari kwani hakuna mfungwa au maabusu aliyelalamika kupitilizwa muda wa siku 90 wa kusomewa shitaka lake mara wanapowekwa vizuizini kwa mujibu wa sheria.

Ilipofika wakati wa maswali, wafungwa na mahabusu walianza kwa kubainisha changamoto zao wanazokumbana nazo kupitia risala iliyosomwa na Mahabusu Michael Marko ambayo pamoja na mengine ilielezea changamoto ya ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi unakopelekea mrudikano wa mahabusu gerezani, Ucheleweshwaji wan akala za hukumu kwa watu ambao wameshahukumiwa, Kuporwa fedha wakati wakikamatwa na polisi na pia wakasema kumekuwa na kawaida ya mahabusu kukamatwa na kuachiwa huku pia wakiituhumu Ofisi ya Mashtaka kutokuleta mashahidi kwa wakati.

Hali ikazidi kubadilika mara baada ya wafungwa na mahabusu hao kupewa nafasi ambapo bila kusita wala uoga waliwataja maaskali na maofisa upelelezi pamoja na makarani wa mahakama kwa majina ambao waliwapora fedha wakati wakikamatwa na wengine kuwataka walipe ili kesi zao zisiendelee. Na pia mahabusu na wafungwa hao walieleza kuwa walitakiwa kutoa hela zilizoanzia milioni mbili na kuendelea ili waachiwe wakati mahabusu mwingine akidai askari alimwambia mke wake atoke Singida aje alale Manyara na siku ya pili mumewe ataachiwa (Akiashiria rushwa ya ngono).

Baada ya kupokea malalamiko hayo, Naibu Waziri aliwaagiza viongozi wa polisi pamoja na wa Ofisi ya Mashtaka alioambatana nao kuhakikisha kuwa wale wote waliotajwa katika tuhuma hizo uchunguzi wa kina unafanyika na wale wote watakaobainika kuwa wametumia mamlaka yaka yao vibaya basi hatua kali za sheria zichukuliwe dhidi yao na pia akawaagiza viongozi ha kuhakikisha wana jitihada za upatikanaji wa haki kwa mahabusu na wafungwa hao unapatika kwa wakati na bila usumbufu.



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul akisikiliza kesi ya mahabusu Mwajuma Mado aliyefika gerezani hapo ikiwa ni sehemu ya msaada unaotolewa na timu hiyo kwa watu walio vizuizini.*



*Timu ya wataalamu na uongozi wa gereza wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza kazi hiyo ya kutoa msaada wa kisheria kwa watu walio vizuizini.*



CamScanner

# MSLAC YAMALIZA MGOGORO WA ARDHI ULIODUMU MIAKA 10 KITETO

**Na Lusajo Mwakabuku & George Mollel - WKS Kiteto**



*Bibi Elizabeth Mungure na Bwana Mwarabu Kitisha wakipeana mikono ikiwa ni ishara ya kumaliza mgogoro wao uliodumu kwa muda wa miaka 10 huku wakishuhudiwa na Viongozi wa Kijiji, Wazee wa kimila na wataalam wa MSLAC tarehe 30/05/2023.*

Timu ya wataalam wanaotekeleza Mama Samia Legal Aid Campaign (MSLAC) katika Mkoa wa Manyara, wilayani Kiteto, imefika katika Kijiji cha Mbigiri na kumaliza mgogoro uliodumu kwa miaka 10 kati ya Bibi Elizabeth Mungure na Bwana Mwarabu Kitisha ambao kwa pamoja walikubaliana kumaliza tofauti zao kwa kutoendeleza shauri hilo mahakamani.

Usuluhishi wa Mgogoro huo uliochukua takribani masaa manne ukihusisha viongozi wa Kijiji pamoja na wazee wa kimila ulifanyika siku ya tarehe 30/05/2023 ambapo pande zote mbili zilizokuwa zinavutana ziliridhia kuwa mgogoro huo uishe kwa makubaliano kwamba Mzee Mwarabu aondoke yeye na mifugo yake katika eneo hilo ifikapo Julai 2023 na Bi. Mungure aondoe kesi hiyo mahakamani.

Kesi hiyo licha ya kuchukua muda mrefu lakini pia ilifika hadi ngazi ya Mahakama Kuu na ikaonekana irudi ianze upya katika ngazi ya Kijiji. Wakati hilo likitekelezwa, ndipo kamati ya wataalam wa Mama Samia Legal Aid Campaign ilifika katika Kijiji hicho na Mwenyekiti wa Kijiji pamoja na mambo mengine akawaelezea wataalam hao juu ya mgogoro huo na kuwaomba kuona namna ya kuumaliza.

Kabla ya kuanza kutafuta suluhisho kuhusu mgogoro huo, timu ya wataalam wa MSLAC ilitoa elimu kwa ufupi juu ya umuhimu wa kumaliza migogoro kwa njia mbadala ikiwemo usuluhishi kwani njia hii hutumia gharama ndogo lakini pia hufanyika eneo husika tofauti na kesi inapopelekwa mahakamani ambapo wahusika hulazimika kupoteza muda mwingi kuhudhuria katika kusikiliza mashauri mahakamani muda ambao wangekuwa wakiutumia kwa ajili ya maendeleo yao binafsi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Baada ya elimu hiyo, timu ikafanya ziara ya kukagua mipaka ikiwa na pande zote mbili zenye mgogoro ambapo wakafanikiwa kuongea na uongozi wa Kijiji uliopo na uliotangulia (Wastaafu) na pia wazee wa kimila walioishi eneo hilo kwa muda mrefu ambapo kwa pamoja walifanya majadiliano na mapendekezo yakafanyika yaliyopelekea kumaliza mgogoro huo.

Baada ya pande zote mbili kuridhia suluhisho hilo lililosimamiwa na wataalamu wa MSLAC, wawili hao walishikana mikono ikiwa ni ishara ya kumaliza tofauti zao juu ya huo mgogoro na kuruhusu amani itawale na wazee wa kimila wakiongozwa na mzee wa ukoo bwana Mbembile Oleikurkur wakawaapisha ili wasiendelee na mgogoro huo.

Timu ya MSLAC imekamilisha kazi ya kutoa huduma ya msaada wa kisheria Mkoani Manyara siku ya tarehe 01/06/2023 na inatarajia kuendelea na kazi hiyo katika mkoa wa Shinyanga kuanzia tarehe 12 – 22 ya mwezi wa Julai mwaka huu. Huduma zinazotolewa ni pamoja na elimu ya sheria za mirathi, migogoro ya ardhi, ukatili wa kijinsia, na kutatua kero mbalimbali zinazohusu masuala ya kisheria.



*Kikao cha usuluhishi wa kesi ya Bibi Elizabeth Mungure na Bwana Mwarabu Kitisha kilichochukua zaidi ya saa nne kikiendelea kijijini Mbigiri, wilayani Kiteto tarehe 30/05/2023.*



CamScanner

# MAMA SAMA LEGAL AID CAMPAIGN YAKUTANA NA WATOTO WA SHULE YA MSINGI WANAOJIHUSISHA NA VITENDO VYA ULAWITI - MANYARA.



*Wakili Eliakim Paul kutoka Civic Social Protection Foundation (CSP) akitoa ushauri nasaa kwa mtoto mwenye umri wa miaka nane ambaye alibainika na kukiri kujihusisha na vitendo vya ulawiti.*

## Na Lusajo Mwakabuku – WKS Manyara

Ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa kampeni ya msaada wa kisheria maarufu kama Mama Samia Legal Aid Campaign Mkoani Manyara, timu ya wataalam ilifika katika Kata ya Maisaka katika mtaa wa Sinai Wilayani Babati ambapo pamoja na kuongea na Wananchi wa eneo hilo, timu hiyo ilipata wasaa wa kuzungumza na Walimu pamoja na kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Sinai tarehe 24/05/2023.

Katika mazungumzo hayo mwalimu wa maadili Bi. Theresia Josephat akawaambia wataalam hao kuwa kulikuwa na watoto kadhaa walioonekana kuwa watoro sugu na baada ya kuwafuatilia, mwalimu huyo akabaini kuwa watoto hao waliishia kukaa kwenye vichaka na majumba mabovu. Baada ya kuwabana kuwa huwa wanafanya nini ndipo walipokiri kuwa walikuwa wanafanya vitendo vya kulawitiana walivyofundishwa na kijana anayesoma kidato cha kwanza.

"Watoto waliofanyiwa ukatili huo walikuwa ni wanafunzi watoro, wakati wa kufuatilia hao wanafunzi watoro ndipo tukabaini kuwa walikuwa wakitoka nyumbani lakini hawafiki shule wanaishia kwenye vichaka huko maporini na majumba mabovu ambapo wamekuwa wakifanya vitendo hivyo vya kulawitiana" alisema Mwalimu Theresia.



*Mawakili na wataalam wa Mama Samia Legal Aid Campaign wakiendelea kutoa elimu kwa Watoto waliokiri kujihusisha na vitendo vya ulawiti.*

Aidha, baada ya kupata taarifa hizo, uongozi wa shule ulipeleka suala hili katika dawati la jinsia la Polisi ambapo walishauriwa kuwapeleka watoto hao hospitali wakapimwe ili ijulikanae kama ni kweli wanajihusisha na kuingiliana kinyume na maumbile hata hivyo baada ya kupimwa hapakuwa na ushahidi wa kutosha kwani watoto hao wanaoshiriki vitendo hivyo bado ni wadogo hivyo jukumu hilo likarudi kwa uongozi wa shule katika kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa shuleni hapo.

Taarifa hiyo ilipelekea wataalam hao kutoa elimu ya ujumla juu ya masuala ya ukatili wa kijinsia na namna za kujilinda na masuala ya kujamiiana ikiwa ni pamoja na kutumia wimbo wa "Don't Touch" unaoelezea maeneo mbalimbali ya mwili ambayo mtoto haruhusiwi kumruhusu mtu yeyote kugusa na kuwahimiza kutoa taarifa kwa mwalimu au Mzazi au kupiga simu namba 116 kwa msaada wa haraka mara anapojitokeza mtu atakayetaka kuwagusa maeneo yao ya siri.

Baada ya Elimu hiyo, wataalam wakatenga muda wa kuongea na watoto waliojihusisha na vitendo hivyo vya kulawitiana kwa kuita mtoto mmoja mmoja ambapo wote walikiri kushiriki katika vitendo hivyo na wakawapa ushahuri nasaa kwa wote walioathirika na vitendo hivyo.

Mwalimu Theresea akatoa rai kwa wazazi kuhakikisha kuwa wanawachunguza watoto wao mara kwa mara kwani walipowaita wazazi wa watoto hao watoro, wazazi walionekana kutokujua lolote kuhusu maendeleo ya kielimu kwa watoto wao na hivyo wakawashauri wahakikishe wanawafuatilia kwani Watoto hao walikuwa hawafiki shule, wanafanyiwa vitendo vya ulawiti hata maeneo ya nyumbani na maendeleo yao kimasomo ni mabaya lakini wazazi hawana taarifa.

Kampeni hii inafanyika kwa siku kumi Mkoani Manyara katika majimbo yote Saba ambapo wataalam wa Sheria kutoka Serikalini na Taasisi binafsi wameungana kwa pamoja katika kuhakikisha kuwa maono ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanafikiwa katika kuhakikisha watu wanyonge na walio pembezoni wanafikiwa na msaada wa kisheria.



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul akiuliza swali kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Sinai juu ya haki zao.*



*Mtaalam wa Sheria kutoka Wizara ya Katiba na Sheria Bwana Laurent Burilo akiimba na wanafunzi wa shule ya Msingi Sinai wimbo wa "Don't Touch" huku akionesha maeneo ambayo wanafunzi hawaruhusiwi kuruhusu yaguswe.*



*Mwalimu Theresia Josephat aliyewabaini watoto watoro sugu na baada ya kuwafuatilia, na kubaini kuwa watoto hao walikuwa wakijificha kwenye vichaka na majumba mabovu walikuwa wanajihusisha na vitendo vya ulawiti.*



CamScanner



Wataalamu kutoka Wizara ya Katiba na Sheria wakiwa na Mbunge wa Mbulu Vijijini Flatei Massay (Mwenye Kaunda Suti) baada ya Wataalam hao kufika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwa ajili ya kutoa Elimu ya Msaada wa kisheria katika Halmashauri hiyo

# Mbulu wajitokeza kuipokea Mama Samia Legal Aid Campaign

**Na George Mwakyembe**

Mama Samia Legal Aid Campain imepokelewa kwa mwitikio mkubwa na wananchi mbalimbali wa wilaya hiyo wakiwemo wakazi wa kata Dinamu wilayani Mbulu ambao wamejitokeza kwa wingi katika viwanja vya kijiji cha Muslur kwa lengo la kuwasikiliza watalaam kutoka Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi mbalimbali zinazoshiriki katika kampeni hiyo.

Wakiongea katika nyakati tofauti, wananchi hao walisema kampeni hiyo imekuja wakati muafaka kwani kuna mambo mengine ambayo wao walikuwa wakiyafanya wakiamini kuwa hiyo ndivyo inavyotakiwa kuwa bila kujua kuwa ni unyanyasaji wa kijinsia hasa masuala ya ndoa na wanawake kumiliki mali ambapo mara zote upendeleo umekuwa kwa mtoto wa kiume au mwanaume.

Vilevile Wananchi ho wamemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwaletea kampeni hiyo ambayo imekuwa msaada mkubwa katika kutatua migogoro ya ardhi kwani wengi wao walikuwa wanashindana kwa maneno na vitisho huku wale waliopelekewa kuamua kesi hizo wakiwa na uwezo mdogo wa kutatua kero hizo.

Kwa upande wake Mbunge wa Mbulu Vijijini Mhe. Frateli Masai amewataka wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wataalam wa kampeni hiyo ikiwa ni pamoja na kutoficha matatizo yaliyopo katika jamaii yakiwemo ukatili wa kijinsia na pia akawataka wananchi kuhakikisha wanajitokeza kwa lengo la kupata elimu kuhusiana na masuala ya unyang'anyi wa ardhi unaopelekea kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kwenye jimbo hilo.



Wakazi wa Kata ya Dinamu Halmashauri ya Wilaya Mbulu Mkoani Manyara wakiwa wanawasikiliza wataalam kutoka Wizara ya Katiba na sheria hawapo pichani walipokuwa wakitoa Msaada kuhusu ukatili wa kijinsia Kupitia kampeni ya Mama samia Legal Aid ambayo inaendelea Mkoani Manyara kwa siku 10 kuanzia tarehe 23 Mei 2023 hadi 01 Juni 2023.



Mwanasheria kutoka wizara ya katiba na sheria Bi. Agnes Mkawe akizungumza na wakati wa kata ya dinamu alipokuwa akitoa msaada wa kisheria kupitia kampeni ya Mama Samia Legal Aid Wilayani Mbulu Mkoa wa Manyara.

"Hii ni nafasi ya kipekee kwetu sisi hasa ukichukulia kuwa Mkoa wa Manyara umekuwa ni mkoa wa pili katika kupata huduma hii toka ilipozinduliwa rasmi utekelezaji wake pale Dodoma tarehe 27/04/2023, hivyo tumepata upendeleo wa Rais wetu mpendwa basi tujitahidi kuhakikisha kuwa tunajitokeza kwa wingi kupata elimu hii ili tuweze kupunguza kama sio kumaliza kabisa hii migogoro ya ardhi pamoja na ukatili wa kijinsia hasa katika masuala ya ukeketaji" alisema Mhe. Masai.

Kampeni ya Mama Samia Legal Aid inatolewa katika Halmashauri zote saba za mkoa wa Manayara na itachukua siku kumi kuanzia tarehe 24 Mei mpaka tarehe 1 Juni 2023.



CS CamScanner

# Habari katika picha

Viongozi na wabunge walioshiriki uzinduzi wa kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign) wakitoa salamu kabla ya uzinduzi huo rasmi.



MAMA SAMIA Legal Aid Campaign



Wataalam wa Mama Samia Legal Aid Campaign wakiendelea kutoa huduma kwa wananchi katika viwanja vya Stendi ya zamani mjini Babati



MAMA SAMIA Legal Aid Campaign

CS CamScanner




Wizara ya Katiba na Sheria kupitia Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu – RITA iliweza kusajili vizazi na vifo, talaka na ndoa pamoja na kutoa elimu ya namna ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu na kushughulikia mirathi.




MAMA SAMIA
Legal Aid
Campaign

CS CamScanner




CS CamScanner




CS CamScanner




MAMA SAMIA Legal Aid Campaign

CamScanner





MAMA SAMIA
Legal Aid
Campaign

CamScanner




CamScanner

# MAJIBU NA MASWALI




CamScanner




CamScanner





MAMA SAMIA
Legal Aid
Campaign

CS CamScanner